# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# SHULE YA SEKONDARI ILBORU

**Simu: 0754985022** **S. L. P 3014,**
**ARUSHA**

**MAWASILIANO**
**MKUU WA SHULE: 0621740533 / 0754985022**
**MAKAMU MKUU WA SHULE: 0767032368/ 0762162689**
**WALIMU MALEZI: 0782720622/ 0764830960/0754090978**
**MZAZI/MLEZI WA: ………………………………………………….**
**S.L.P:…………………………………………….**
**…………………………………………………**

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI ILBORU HALMASHAURI YA ARUSHA MKOA WA ARUSHA MWAKA- 2026</u>**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga katika shule hii ya sekondari Ilboru kwa mwaka 2026.

Shule hii ni maalum kwa maana ya mahali pa kusomea vijana wa kiume wenye ufaulu wa hali ya juu. Kwa mantiki hiyo mwanafunzi atatakiwa asome kwa bidii na awe na nidhamu ya hali ya juu kwake mwenyewe, kwa wanafunzi wenzake, walimu ,wafanyakazi wengine, wageni pamoja na nidhamu ya kujituma kwa bidii wakati wote awapo shuleni.

Aidha mwanafunzi anapaswa kuelewa kwamba serikali imempatia nafasi katika shule hii kwa lengo la kuandaliwa kulitumikia taifa letu kama mtaalamu bingwa na mzalendo huku akiishi kwa motto wa shule "**ELIMU KWA HUDUMA"**

Shule ya Ilboru iko umbali wa kilometa mbili kaskazini mwa mji wa Arusha.

Usafiri wa taxi ,bajaji au pikipiki(BODABODA) kutoka mjini unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi.Nauli ni shillingi 15,000/= kwa taxi,5,000/= kwa bajaji na 3,000/= kwa bodaboda.

Mhula wa masomo utaanza .........2026, hivyo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe .........2026 mpaka tarehe ..............2026.

**Mambo muhimu ya kuzingatia;**

1. **Sare za shule.**
   - (i) Mashati mawili meupe (tetron) ya mikono mifupi
   - (ii) Suruali mbili nyeusi – (zenye marinda mawili)
   - (iii) Nguo za ndani za kutosha,
   - (iv) Tai nyeusi mbili (2) yenye nembo ya shule ( Zinapatikana duka la shule)
   - (v) Viatu vya ngozi vyeusi jozi moja au zaidi vya kufunga kwa kamba. Visiwe na kisigino kirefu.
   - (vi) Madaftari 12 (Counter), graph paper pads (02).
   - (vii) Mathematical Set, Ream paper $A_4$ moja (1) kwa kila muhula, Kalamu zisizopungua 05, Na penseli za kutosha.
   - (viii) Tshirts mbili za rangi ya light blue zenye nembo ya shule. (Zinapatikana duka la shule)
   - (ix) Track suit za rangi ya kijivu zenye nembo ya shule. (Zinapatikana duka la shule)
   - (x) Raba jozi moja (flat), bukta (kaptula ya michezo) dark green na T-shirt green kwa ajili ya michezo mikono mifupi(jezi)(zisizo na maandishi)
   - (xi) Soksi nyeusi jozi nne au zaidi.
   - (xii) Mto na foronya (Light blue).
   - (xiii) Taulo
   - (xiv) Godoro la Sponji (futi 2½).(Litapatikana duka la shule)
   - (xv) Shuka mbili (light blue) na blanketi moja (au mbili ukijiweza)
   - (xvi) Ndoo mbili (2) za Maji za lita 10.
   - (xvii) Tranker (Sanduku la bati); asije na la mbao.
   - (xviii) Kijiko, sahani, bakuli na kikombe (½ lita)
   - (xix) Aje na Picha (Passport size) moja ya mzazi/mlezi,moja ya mwanafunzi na nyingine ya ndugu wa karibu alio nao.
   - (xx) Mahitaji ya kibinadamu (sabuni za kufulia na kuogea, sabuni ya maji (Disinfectant) lita 5, dawa ya meno, mswaki, chanuo, kioo, n.k)
   - (xxi) Mkanda mweusi wa ngozi wa suruali.
   - (xxii) Sweta nyeusi moja au zaidi yenye nembo ya shule. (Zinapatikana duka la shule)
   - (xxiii) Begi la kubebea madaftari
   - (xxiv) Suruali rangi ya kijivu cheusi. (Kama rangi itakuchanganya uje ushonee shuleni).
   - (xxv) Vifaa vya usafi : Soft Broom (2), Hard Broom (2), Squizer (2), Chelewa (2) yenye mpini, Toilet brush(2), jembe lenye mpini 1.

**Mwanafunzi asije na nguo yoyote tofauti na sare zilizoagizwa.**

1. Kitambulisho kitapatikana shuleni.

**Simu za mikononi, line, Heater na pasi ya umeme, redio , charger na vifaa vinavyotumia umeme, haviruhusiwi kabisa hapa shuleni. Atakayekamatwa navyo atafukuzwa shule mara moja.**

(i) **Kutakuwa na Ukaguzi siku ya kuripoti Shuleni, na ukaguzi wa dharura wakati wowote.**

(ii) **Mzazi atoe Namba yake ya simu kwa mawasiliano ya haraka kupitia Ofisi ya Mkuu wa Shule na katika fomu ya maelezo binafsi iliyoambatanishwa.**

- Ni lazima kila mwanafunzi awe na bima ya afya, kama hana aje na Tsh 50,400/= ili akatiwe bima ya afya.

**NYARAKA ZA KUKABIDHI**

1. **Cheti cha Daktari:**

   Hapa imeambatanishwa fomu ambayo lazima Daktari wa Hospitali ya Serikali athibitishe hali yako ya afya na kwamba unaweza kumudu masomo yako vizuri. Hivyo hakikisha unapimwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali (sio kituo cha afya) kabla ya kufika hapa shuleni na fomu hiyo kuiwakilisha hapa shuleni mara tu unapofika.

2. **Unatakiwa kuja na kivuli cha Fomu ya kuzaliwa au Birth Certificate.**

3. **Fomu ya kukubali Masharti ya Shule:**
   **Shule hii ni ya Serikali hivyo haina dini. Kwa mwanafunzi mwenye msimamo na mhemko mkali wa kidini, mzazi anashauriwa ampeleke shule za Seminari.**

**N.B:** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
Ninakutakia safari njema ya kuja hapa shuleni.

- **Muda wa Mwisho wa kupokelewa shuleni ni saa 11: 30 jioni.**

Karibu sana.

DENNIS J. OTIENO
MKUU WA SHULE
THE HEADMASTER
ILBORU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box [illegible] ARUSHA

## SHERIA ZA SHULE

Tabia njema ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya hafai kupewa Elimu ya Sekondari au Elimu ya juu. Ni lazima mwanafunzi awe na tabia nzuri wakati wote. Kila mwanafunzi analazimika kutii sheria za shule na kufuata taratibu za shule, pia kuwatii wafanyakazi na walimu na wengine wenye mamlaka. Heshima na adabu kwa mtu yeyote ni kitu cha lazima.

## SHERIA ZA JUMLA:

1. Kunywa pombe au kuvuta sigara au kiko ni mwiko.
2. Uzinifu wa aina yoyote ni kosa kubwa sana.
3. Kila mwanafunzi ni lazima awe mtiifu kwa walimu wake wote, wafanyakazi wote, makaka wa shule wote, na wakuu wengine wote. Ujeuri au ubishi wa aina yoyote kwa mwalimu, kaka wa shule au wakuu wengine wote ni mwiko.
4. Hakuna mwanafunzi yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya maeneo ya shule, bila ruhusa (pass) toka kwa mwalimu wa zamu, isipokuwa siku ya kuruhusiwa kwenda mjini rasmi (town leave). Mwalimu au kaka wa shule akimwona mwanafunzi yeyote mjini ana haki ya kumwomba amwonyeshe cheti cha ruhusa (pass).
5. Ruhusa ya kulala nje ya shule, itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu wake tu.
6. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zote ikiwa ni pamoja na bustani, usafi kama vile anavyopaswa kuheshimu masomo ya darasani.
7. Matusi ya aina yoyote, yawe ya kusema au kuandika hayaruhusiwi shuleni.
8. Kila mwanafunzi lazima aheshimu na kutunza mali ya shule, uharibifu wowote utakaotokea utabidi ugharimiwe na mwanafunzi mwenyewe.
9. Sare za shule (uniform) ni lazima zivaliwe wakati wa masomo na wakati wa kuruhusiwa kwenda mjini. Hakuna mwanafunzi yeyote atakayeruhusiwa kutoka nje ya mipaka ya shule bila kuvaa sare za shule, isipokuwa tu kama ruhusa rasmi imetolewa na Mkuu wa Shule.
10. Wizi wowote hauruhusiwi shuleni, iwe ni wa mali ya shule au mali ya mwanafunzi au mfanyakazi.
11. Usafi wa mwili, mavazi, madarasa, mabweni, jumba la chakula (dining hall) jumba la mikutano (assembly hall) jumba la mihadhara (lecture hall) viwanja ni wajibu wa kila mwanafunzi.
12. Ugomvi wa maneno au kupigana ni mwiko shuleni.
13. Kuchelewa kwa aina yoyote bila ruhusa ni kosa, mfano kuchelewa toka mjini, wakati wa roll-call, kuchelewa inspection na kuchelewa toka likizo.
14. Tabia njema shuleni na nje ya shule ni wajibu na ni lazima kwa kila mwanafunzi.
15. Taa za shule na maji ya shule lazima vitumiwe kwa uangalifu.
16. Magazeti au vitabu vyenye picha au maneno yasiyofaa havitakiwi shuleni.
17. Upokeaji au uandishi wa maneno yasiyofaa ni mwiko shuleni.
18. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kuandika barua yoyote kwa Mkuu yeyote mahali popote ya kiofisi bila ya kuipitisha kwa Mkuu wa Shule (k.k. Mkuu wa Shule).
19. Mwanafunzi yeyote haruhusiwe kwenda nyumbani kwa Mwalimu au Mfanyakazi yeyote bila ruhusa ya mwalimu anayehusika.

20. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutumia vyombo vinavyotumia umeme kama vile redio, heater, pasi, earphone n.k. mabwenini au kufanya ufundi wa aina yoyote kwenye umeme bwenini au darasani.
21. Ili kuepukana na utoro, kofia polinek na majaket **haziruhusiwi** hapa shuleni.
22. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani pamoja na 'night preparation'
23. Ni kosa kupiga kelele Smart Area.
24. Ni kosa kugomea mitihani ya ndani na nje.
25. Utahudhuria mchakamchaka kwa muda na siku zote zilizopangwa na shule bila kukosa.
26. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini akiwa shuleni bila ridhaa ya mzazi kwa maandishi.

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule mara moja:**

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vila uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.

(e) Kupigana au kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuoa au kuolewa

(i) Kushiriki kutoa mimba.

(j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

(k) Kukataa adhabu kwa makusudi

(l) Kuwa na simu ya mkononi au line ya simu, Charger, Flash, CD, Heater, Pasi ya umeme na kifaa chochote kinachotumia umeme.

(m) Kulala nje ya shule bila ruhusa.

(n) Kutoroka kwenda nje ya shule, kuhudhuria kumbi za starehe kama Club za disco, bar na kubert (kucheza kamali), kwa aina yoyote.

…..........................

…….......................

….........................

Tarehe …….........

Mkuu wa Shule,
Ilboru Sekondari,
S.L.P. 3014,
**ARUSHA.**

**YAH: <u>KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ILBORU</u>**

Nachukua nafasi hii kulishukuru Taifa letu kwa kunichagua na kunipa nafasi ya kupata Elimu ya Sekonari. Hii ni bahati kubwa na ninaahidi kujifunza kadiri ya uwezo wangu na sitapoteza muda wa masomo darasani au muda wa kazi za mikono kwa kuwa mvivu, au kupuuza shughuli hizo.
Nimesoma sheria za shule na masharti ya kujiunga na shule ya Sekondari Ilboru na ninakuthibitishia kuwa nimeafiki sheria na masharti hayo na kwamba nitaziheshimu kwa kutokuzivunja kwa makusudi. Na ikiwa nimezivunja ninastahili kuadhibiwa **vikali.**

Wako mwanafunzi mtiifu,

……………………………….
Jina na Sahihi ya Mwanafunzi

……………………………….
Jina na Sahihi ya Mzazi/Mlezi

*NB: (i) Wasilisha fomu hii kwa Mkuu wa Shule mara tu ufikapo shuleni ili iwekwe kwenye jalada lako.*

**MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING**

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

***(To be completed by a medical Officer in respect of all form I and 5 entrants)***

Pupil's full name ……………………………………………………………………………………………

Age ……………………………………………………………………………………………………

Blood count (red and white) …………………………………………………………………………

Stool examinations …………………………………………………………………………………

Urinalysis ……………………………………………………………………………………………
Syphilis test …………………………………………………………………………………………
T.B.test…………………………………………………………………………………………………
Eye test ………………………………………………………………………………………………
Ears ……………………………………………………………………………………………………
Chest……………………………………………………………………………………………………

Abdomen………………………………………………………………………………………………

Spleen…………………………………………………………………………………………………

Additional information: e.g. physical defects, infection, chronic or family diseases etc.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further studies.

Signature ………………………………

Designation ………………………………

Station ………………………………

Date: ………………………………

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. JINA …………………………………………………. DINI ………………………………………….

2. TAREHE YA KUZALIWA……………………………3. KIJIJI ULIMOZALIWA……………………..

4. TARAFA ULIMOZALIWA ……………… ...5. WILAYA ULIMOZALIWA ……………………

6. MKOA ULIMOZALIWA …………………………. KAMA UNAKAA MJINI…………………..

7. TAJA MJI… MTAA………………..BARABARA……………………….

8. JINA LA BABA……………………………..9. KAZI YA BABA………………………………

10. ANWANI YA BABA……………………………………………………………………………

11. JINA LA MAMA ………………………………. 12. KAZI YA MAMA…………………………………

13. ANWANI YA MAMA…………………………………………………………………….

14. JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:

JINA:……………………………………………………

ANWANI:………………………………………………………….

SIMU:………………………………………………. EMAIL:………………………… .

15. SHULE ULIZOSOMA MADARASA MADARAKA ULIYOSHIKA

| SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA |
|---|---|---|
| ……………………………. | ………………… | ………………………………… |
| ……………………………. | ………………… | ………………………………… |

16. JE, BABA YU HAI? …………………………………. (NDIYO/HAPANA)

17. JE, MAMA YU HAI? …………………………………. (NDIYO/HAPANA)

18. JE, UNAKAA NA MLEZI ……………………………. (NDIYO/HAPANA)

19. ANWANI YA MLEZI ………………………………………………………………………

20. KAZI YA MLEZI …………………………………………………………………………

21. ELEZA MATATIZO YA NYUMBANI, YA MAGONJWA, N.K. YANAYOKUKABILI

……………………………………………………………………………………………………

22. UNAFIKIRI MATATIZO HAYO YATATATULIWA VIPI?

……………………………………………………………………………………………

23. ELEZA MIPANGO YAKO YA MAISHA YA BAADAYE

……………………………………………………………………………………………………

24. MKO WANGAPI KATIKA FAMILIA? (A) WA KIUME ……………………………………

(B) WA KIKE ……………………. (C) WEWE NI WA NGAPI ………………………………

(D) NDUGU WANGAPI WAMEAJIRIWA? ……………………………………………………

25. KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

…………………………………………………………………………………………………

26. KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

…………………………………………………………………………………………………

27. JINA ………………………………… SAHIHI……………… TAREHE…………………………

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Ukiwa mwanafunzi na mzazi/mlezi wamekubaliana na masharti yote ya shule, sharti fomu hii isainiwe na watu wanne, ambao ni:

(i) Mwanafunzi mwenyewe: Jina kamili ____________________
Kidato ___Saini_______Tarehe_______

(ii) Mzazi/Mlezi: Jina kamili
__________________________Saini_______________Tarehe________

(iii) Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa: Jina la Kijiji/Mtaa
____________________________________

Jina la Afisa Mtaa/Kijiji:
__________________________________________________

Maoni/Mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu:

-----------------------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------------

Saini ya Afisa Mtendaji ________________________________ Tarehe _______________

Mhuri wa Afisa Mtendaji:

(iv) Mtendaji Kata/Mtaa: Jina la Kata/Mtaa
___________________________________

Jina la Afisa Mtendaji Kata/Mtaa ___________________________

Saini ya Afisa Mtendaji Kata ___________________________ tarehe ____________

Mhuri wa Afisa Mtendaji Kata:

**VITABU VILIVYOPENDEKEZWA KWA AJILI YA KIDATO CHA KWANZA**

1. **MATHEMATICS**
   Mathematics for secondary school book one-TIE
   -Mathematics for secondary school book one -OXFORD

2. **ENGLISH LANGUAGE**
   English for Secondary School Book one- Tanzania institute of education (TIE)

   Students Dictionary for learners using English to study other subjects 3rd Edition.

3. **PHYSICS:**
   Physics for secondary school book one—Tanzania institute of education (TIE)

4. **CHEMISTRY:**
   Chemistry for Sec. School Book one– Tanzania institute of education (TIE)
5. **KISWAHILI:**
   Kiswahili Kidato cha Kwanza- Tanzania institute of education (TIE)
6. **GEOGRAPHY:**
   - Geography for Sec. School Bk. I, Tanzania institute of education (TIE)

7. **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**
   Historia ya Tanzania na maadilili kidato cha kwanza: Tanzania institute of education (TIE)

8. **BUSINESS STUDIES**
   Business studies for Secondary School BK. I –. Tanzania institute of education (TIE)

9. **BIOLOGY** Biology for secondary school book 1-- Tanzania institute of education (TIE)

10. **CHINESE LANGUAGE:** for secondary school book 1: Tanzania institute of education (TIE)

**NB**: Mzazi unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu vilivyopendekezwa hapo juu kwa matumizi yake binafsi.

## FOMU YA KUTOKUWA NA SIMU PAMOJA NA VIFAA VINAVYOTUMIA UMEME.

Mimi mwanafunzi....................................................................................................

wa Ilboru Sekondari nimesoma na kuelewa sheria zote za shule....................................

Nakiri niwapo shuleni muda wote sitamiliki wala kutumia simu ya mkononi au kifaa chochote kinachotumia umeme. Hivyo basi endapo nitakamatwa navyo nifukuzwe shule mara moja.

Sahihi ya mzazi.......................................................

Jina la mwanafunzi..................................................

Tarehe..............mwezi..................mwaka...............

Mzazi wa.................................................................

Nimesoma na kuelewa sheria za shule na ukiri wa mwanangu kutii na kufuata sheria na taratibu za shule na hasa umiliki na matumizi ya simu na vifaa vya umeme.

Endapo atakamatwa/kukutwa na simu au vifaa vya umeme, afukuzwe shule mara moja.

Sahihi ya mzazi.......................................................

Jina la mzazi...........................................................

Tarehe..............mwezi..................mwaka...............